

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**MKUTANO WA SABA**

**YATOKANAYO NA KIKAO CHA ISHIRINI NA TISA**

**19 MEI, 2017**

## **MKUTANO WA SABA**

### **KIKAO CHA ISHIRINI NA TISA TAREHE 19 MEI, 2017**

#### **I. DUA:**

Naibu Spika Mhe. Tulia Ackson alisoma Dua na kuongoza Bunge Saa 3:00 asubuhi.

#### **Makatibu mezani:**

1. Ndugu Theonest Ruhilabake
2. Ndugu Neema Msangi

#### **II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

##### **Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani:-**

- (1) Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi aliwasilisha:-

Hotuba za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

- (2) Mhe. Mattar Ali Salum – (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji aliwasilisha Mezani:

Taarifa ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 pamoja na maoni ya Kamati juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

- (3) Mhe. Susan A. J. Lyimo – Msemaji Mkuu wa Upinzani kwa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi aliwasilisha Mezani:-

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, juu ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

### **III. MASWALI**

#### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI)**

Swali Na. 234: Mhe. Cosato D. Chumi

Nyongeza: Mhe. Cosato D. Chumi  
Mhe. Kasuku S. Bilago  
Mhe. Daimu I. Mpakate

#### **WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**

Swali Na. 235: Mhe. Dr. Mary M. Mwanjelwa

Nyongeza: Mhe. Dr. Mary M. Mwanjelwa  
Mhe. Susan A. J. Lyimo  
Mhe. Japhet N. Hasunga

#### **WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI**

Swali Na. 236: Mhe. Yussuf Haji Khamis (kny: Mhe. Mbarouk Salim Ali)

Nyongeza: Mhe. Yussuf Haji Khamis  
Mhe. Roman Selasini  
Mhe. Balozi Adadi Rajab

Swali Na. 237: Mhe. Shally J. Raymond

Nyongeza: Mhe. Shally J. Raymond  
Mhe. Kiteto Koshuma  
Mhe. Dunstan Kitandula

Mhe. Mary D. Muro

## **WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Swali Na. 238: Mhe. Frank Mwakajoka (kny: Mhe. David E. Silinde)

Nyongeza: Mhe. Frank Mwakajoka  
Mhe. Maftah A. Nachuma  
Mhe. Ignas Malocha

Swali Na. 239: Mhe. Halima A. Bulembo

Nyongeza: Mhe. Halima A. Bulembo  
Mhe. Munde T. Abdallah  
Mhe. Kitwana Dau

Swali Na. 240: Mhe. Joseph Mhagama (Kny: Mhe. Jacqueline N. Msongozi)

Nyongeza: Mhe. Joseph Mhagama  
Mhe. Daniel Nsanzugwanko  
Mhe. Susan Mgonokulima  
Mhe. Zaynab Vulu  
Mhe. Rashid Shangazi

## **WIZARA YA AFYA MALIASILI NA UTALII**

Swali Na. 241: Mhe. Alex R. Gashaza

Nyongeza: Mhe. Alex R. Gashaza

## **WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANA'A NA MICHEZO**

Swali Na. 242: Mhe. Devotha M. Minja

Nyongeza: Mhe. Devotha M. Minja

## **WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**

Swali Na. 241: Mhe. Ussi Salum Pondeza

Nyongeza: Mhe. Ussi Salum Pondeza

## **IV. MATANGAZO**

### **A. WAGENI**

1. Wageni wa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Mhe. Dr. Charles Tizeba – Wizara ya Kilimo, wakiongozwa na:-
  - (i) Dkt. Yohana Budeba – Katibu Mkuu (Sekta ya Uvuvi)
  - (ii) Dkt. Maria Mashingo – Katibu Mkuu (Sekta ya Mifugo)
  - (iii) Mhandisi Mathew Mtigumwe – Katibu Mkuu (Sekta ya Kilimo)
  - (iv) Balozi Fred Kafeero – Mwakilishi Mkazi FAO
  - (v) Ndg. Mathayo Mathew – Afisa Mipango kutoka Umoja wa Ulaya (EU)
  - (vi) Ndg. Mohamed Muya – Katibu Mkuu Mstaafu
2. Wenyeviti watatu (3) wa Bodi za Taasisi na Mashirikia yaliyo chini ya Wizara hiyo.

3. Wakurugenzi, Wakuu wa Idara, Taasisi, Vitengo na Maafisa Mbalimbali waliopo chini ya Wizara ya Kilimo.
4. Wageni wa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi – Mhe. Tate Olenasha ambao ni Wapiga kura wake kutoka Jimboni kwake Ngorongoro Mkoa wa Arusha, wakiongozwa na Mhe. Yanick Ngoinyo Diwani wa Kata ya Ololosokwan.
5. Wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge na wanafunzi waliokuja kutembelea Bunge kwa mafunzo.

## **B. KAZI**

1. Mwenyekiti wa Bunge Sports Club – Mhe. William Ngeleja aliwatangazia Wabunge wote kuwa Jumamosi tarehe 20/5/2017 kutakuwa na Michezo ya kirafiki ya football na netball na timu za NSSF katika kiwanja cha Jamhuri saa 10.00 jioni.
2. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais – Mhe. Januari Makamba aliwatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa leo Mhe. Samia Suluhu – Makamu wa Rais, atapokea taarifa kutoka Timu ya Uchunguzi ya Mazingira aliyoiunda kuhusu uchafuzi wa mazingira ya Mto Ruaha.
3. Naibu Spika aliwatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa, kwa kuwa jana tarehe 18/5/2017 Mwenyekiti aliyeongoza Bunge alishatoa pongezi kwa timu ya Serengeti basi hakuna haja tena ya Wabugne kuendelea kupongeza wakati wanapochangia hoja zao.

## **MWONGOZO WA SPIKA**

1. Mhe. Devotha Ninja kwa kutumia Kanuni 68 (7) & 46 alisimama kuomba mwongozo kuhusu kamata kamata ya Waandishi wa Habari wakati wakitekeleza majukumu yao kwamba swali hili la nyongeza halikujibiwa kikamilifu.

Naibu Spika

Alisema atalijibu baada ya kujiridhisha kwenye Hansard. Hivyo Mwongozo huo utajibiwa baadaye.

2. Mhe. Mussa Mbarouk kwa kutumia Kanuni 68 (7) aliomba mwongozo kuhusu utaratibu wa kutambua wageni waliopo gallery za Bunge kwamba wengine kutambuliwa kwa majina na wengine hawatambuliwi hata watokako. Aliomba wageni watajwe japo sehemu wanazotoka, shule au vyuo vyao.

Naibu Spika

Alinukuu Kanuni ya 142 (1) & (2) na kuelekeza kuwa, huo ni uamuzi wa Spika kwa kuzingatia Kanuni hiyo inayompa Mamlaka ya kuamua namna bora ya kutambulisha wageni Bungeni. Hivyo, utaratibu unaotumika sasa ktika kutambua wageni ni kutohana na mwongozo wa Spika uliotolewa wakati wa Briefing.

## V. HOJA ZA SERIKALI

- (1) Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 yaliwasilishwa na Mhe. Waziri.
- (2) Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji – Mhe. Dkt. Mary Nagu aliwasilisha maoni ya Kamati kuhusu Makadieio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.
- (3) Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi aliwasilisha Maoni ya Kambi ya Upinzani ya Wizara hiyo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 (Mhe. Cecilia D. Paresso – alisoma maoni hayo).

Waheshimiwa Wabunge waliendelea kuchangia Hoja ya Bajeti hiyo kama ifuatavyo:-

- |     |                               |   |     |
|-----|-------------------------------|---|-----|
| (1) | Mhe. Dkt. Christine Ishengoma | - | CCM |
| (2) | Mhe. George Mkuchika          | - | CCM |

## **VI. KUSITISHA BUNGE**

Saa 7:00 Bunge mchana lilisitishwa mpaka saa 11:00 jioni.

## **VII. BUNGE KURUDIA**

Saa 11.00 jioni Bunge lilitrudia na Waheshimiwa Wabunge waliendelea kuchangia Bajeti ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kama ifuatavyo:-

- |      |                             |   |         |
|------|-----------------------------|---|---------|
| (3)  | Mhe. Anna K. Malecela       | - | CCM     |
| (4)  | Mhe. Daniel Nsanzugwanko    | - | CCM     |
| (5)  | Mhe. Agness Marwa           | - | CCM     |
| (6)  | Mhe. Daimu I. Mpakate       | - | CCM     |
| (7)  | Mhe. Joseph Haule           | - | CHADEMA |
| (8)  | Mhe. Aida Khenani           | - | CHADEMA |
| (9)  | Mhe. Almas Maige            | - | CCM     |
| (10) | Mhe. Maftah A. Nachuma      | - | CUF     |
| (11) | Mhe. Doto Biteko            | - | CCM     |
| (12) | Mhe. Hamidu Hassan Bobali   | - | CUF     |
| (13) | Mhe. Mbaraka Kitwana Dau    | - | CCM     |
| (14) | Mhe. Elias J. Kwandikwa     | - | CCM     |
| (15) | Mhe. Omar T. Mgumba         | - | CCM     |
| (16) | Mhe. Ignas A. Malocha       | - | CCM     |
| (17) | Mhe. Felister A. Bura       | - | CCM     |
| (18) | Mhe. Constantine J. Kinyasu | - | CCM     |
| (19) | Mhe. Pascal Y. Haonga       | - | CHADEMA |
| (20) | Mhe. Gimbi D. Masaba        | - | CHADEMA |

Mawaziri walianza kuhitimisha hoja mbalimbali za Wabunge kama ifuatavyo:-

1. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvubi – Mhe. William T. Olenasha.
2. Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi – Mhe. Mwigulu L. Nchomba.
3. Waziri wa Nishati na Madini – Waziri wa Nishati na Madini.
4. Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji – Mhe. Charles J. P. Mwijage.

## **VIII. MATANGAZO**

- Naibu Spika alitangaza Semina kuhusu Utalii – Udhibiti wa Mapori itakayoratibiwa na Wizara ya Utalii.
- Naibu Spika pia alijibu Mwongozo wa Mhe. Devotha Minja kuhusu vitendo vyta kuwazuia na kuwaweka ndani Waandishi wa Habari. Kutokana na Hansard majibu ya Nyongeza yalijitosheleza.

## **IX. KUAHIRISHA BUNGE**

Saa 1.45 usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumamosi, Tarehe 20/5/2017 saa 3:00 asubuhi.